

## 22I-Maddul-Far'iy (Ya Matawi) - Maddul-Waajib Al-Muttaswil

### Madd Kutokana Na Hamza:

#### i. مَدُّ الْوَاجِبِ الْمُتَّصِلِ (Maddul-Waajib Al-Muttaswil)

Na inaitwa 'Waajib' kwa kuwa Maqurraa wote wamekubaliana kuivuta zaidi kuliko مَدُّ الطَّبِيعِيِّ (maddutw-twabiy'iy). Na inaitwa 'Muttaswil' kwa kuwepo hamzah na madd katika neno moja. Hukmu yake katika riwaayah ya Hafsw 'an 'Aaswim *twariyq Ash-Shaatwibiyyah* ni kuivuta ima kwa harakah nne au tano.

Mwisho wa neno		Katikati ya neno	
حُنْفَاءَ	السَّمَاءِ	طَائِفَةٌ	لِلْمَلَائِكَةِ
النِّسَاءِ	الْأَنْبِيَاءِ	عَائِلًا	أَوْلَادِكَ
جَاءَ	أَبْتِغَاءَ	وَحَدَائِقَ	الْأَرْبَابِ